**MUSOMA UTALII TRAINING COLLEGE**
P.O. Box 1488 Cell. 0753218140, 0782389825 MUSOMA – MARA –TZ.
Email: admissionmutc@gmail.com Website: www.musomautaliicollege.co.tz

Tarehe 02.09.2023

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Chuo cha Mafunzo Musoma Utalii ni Chuo cha binafsi kilichopo mkoa wa Mara. Kijiografia chuo kinapatikana Musoma mjini jirani na stendi ya mabasi ya mkoa iitwayo Bweri Stendi. Chuo kinatangaza nafasi za kazi katika maeneo ya Food Production, Electrical Installation na Afisa masoko kama ifuatavyo;

(A) MWALIMU-UFUNDI FANI YA *FOOD PRODUCTION* – NAFASI (01)

**MAJUKUMU**

- Kufundisha kozi za *Food Production* na *Tour Guiding* Level I-II kwa mtaala wa NACTVET
- Kusimamia na kuongoza mafunzo kwa vitendo katika kitengo cha Utalii na ukarimu (Tourism and Hospitality)
- Kusimamia ziara mafunzo zinazohusiana na fani za *Food Production*
- Kuwasimamia wanachuo katika muda wote wa mafunzo yao
- Kusimamia kazi za nje za wanachuo katika mafunzo
- Kufanya upimaji na tathimini katika masomo anayofundisha
- Kuwa kielelezo na kuhamasisha tabia njema na maadili ya kitanzania kwa wanachuo
- Kusimamia kazi mradi na kazi za kiutafiti kwa wanachuo
- Kuwasimamia na kuwatahini wanachuo katika mafunzo kwa vitendo
- Kutoa ushauri na nasaha kwa wanachuo kuhusu mienendo ya maisha yao
- Kumshauri mkuu wa chuo kuhusu uboreshaji katika kutoa mafunzo kulingana na utaalamu wa eneo husika

**SIFA ZA MWOMBAJI**

- Awe amesomea kozi ya Food Production au kozi inayohusiana; katika kiwango kisichopungua ngazi ya tatu (Level III) na amefanya kazi katika hoteli au taasisi za kitalii kwa muda usiopungua miaka miwili
- Awe na umahili wa kuzungumza Kiingereza
- Mwenye ujuzi wa kuzungumza lugha nyingine za kigeni kama kifaransa, kijapani, kichina, kikorea n.k atapewa kipaumbele
- Awe na ujuzi wa kutumia kompyuta
- Mwenye cheti cha Ualimu wa VETA atapewa kipaumbele

(B) MWALIMU-UFUNDI FANI YA *ELECTRICAL INSTALLATION* – NAFASI (01)

**MAJUKUMU**

- Kufundisha kozi ya *Electrical Installation* kwa mtaala wa NACTVET
- Kusimamia na kuongoza mafunzo kwa vitendo katika kitengo cha Uhandisi-umeme (Electrical Engineering)
- Kusimamia ziara mafunzo zinazohusiana na fani ya *Electrical Installation*
- Kuwasimamia wanachuo katika muda wote wa mafunzo yao
- Kusimamia kazi za nje za wanachuo katika mafunzo
- Kufanya upimaji na tathimini katika masomo anayofundisha
- Kuwa kielelezo na kuhamasisha tabia njema na maadili ya kitanzania kwa wanachuo
- Kusimamia kazi mradi na kazi za kiutafiti kwa wanachuo
- Kuwasimamia na kuwatahini wanachuo katika mafunzo kwa vitendo
- Kutoa ushauri na nasaha kwa wanachuo kuhusu mienendo ya maisha yao
- Kumshauri mkuu wa chuo kuhusu uboreshaji katika kutoa mafunzo kulingana na utaalamu wa eneo husika

**SIFA ZA MWOMBAJI**

- Awe amesomea kozi ya *Electrical Installation* au kozi inayohusiana; katika kiwango kisichopungua ngazi ya tatu (Level III) na amefanya kazi inayohusiana na fani husika kwa muda usiopungua miaka miwili
- Awe na umahili wa kuzungumza Kiingereza
- Awe na ujuzi wa kutumia kompyuta
- Mwenye cheti cha Ualimu wa VETA atapewa kipaumbele

(C) AFISA MASOKO – NAFASI (20)

**MAJUKUMU**

- Kutembelea shule za sekondari katika maeneo mbalimbali ili kutoa habari kuhusu kozi zinazotolewa na chuo
- Kuchapisha matini mbalimbali mfano matangazo, vipeperushi n.k zenye kueleza taarifa za mafunzo yanayotolewa chuoni kwa wanafunzi na wazazi
- Kusambaza matini mbalimbali za chuo, video na sauti kwaajili ya kutangaza kozi zinazopatikana chuoni
- Kutembelea maeneo yenye mikusanyiko kwaajili ya kukitangaza chuo
- Kufanya mawasiliano ya mara kwa mara na wazazi, wanafunzi na wote waliotuma maombi ya kujiunga na chuo
- Kutembelea ofisi za mashirika na taasisi zinazotoa ufadhili wa kimasomo kwa wanafunzi baada ya elimu ya sekondari ili kutoa taarifa za kozi zinazopatikana chuoni

**MAELEZO YA ZIADA KUHUSU KAZI HII**

- Kazi hii itakuwa ni ya mkataba wa muda (Temporary Contract)
- Msingi wa malipo utafanyika kwa makubaliano ya *kamisheni* katika kila mwanachuo atakayeletwa na Afisa masoko
- Kutakuwa na makubaliano ya gharama za uwezeshaji kwa Afisa masoko wakati akitekeleza majukumu ya kutafuta wanachuo

**SIFA ZA MWOMBAJI**

- Awe mhitimu wa kidato cha nne na zaidi (Wenye Astashahada, Stashahada na Shahada watapewa kipaumbele)
- Awe na ujuzi mkubwa wa stadi za mawasiliano katika kuzungumza na hadhara, kusoma, kuandika na kusikiliza
- Awe na ujuzi na ubunifu wa kutumia mitandao ya kijamii katika matangazo
- Awe ma lugha ya ukarimu kwa wateja (Customer Care)
- Awe na uwezo wa juu wa kuhimili na kuvumilia changamoto za wateja
- Wakazi wa mikoa ya SIMIYU, GEITA, MWANZA, KIGOMA, KAGERA, SINGIDA, KATAVI, RUKWA NA MANYARA watapewa kipaumbele.

**JINSI YA KUTUMA MAOMBI**

- Katika nafasi za MWALIMU-UFUNDI FANI YA *FOOD PRODUCTION* na MWALIMU-UFUNDI FANI YA *ELECTRICAL INSTALLATION* maombi yatumwe kwa Mratibu Mafunzo (Training Coordinator) Chuo cha Mafunzo Musoma Utalii S.L.P 1488- MUSOMA. Maombi yahusishe barua, wasifu binafsi, vyeti vya taaluma na cheti cha kuzaliwa vilivyo katika muundo wa PDF na vitumwe kupitia barua pepe/e-mail ya admissionmutc@gmail.com au jajimaguru@gmail.com . Kichwa cha habari cha barua pepe/e-mail kitaje nafasi husika.
- Katika nafasi ya Afisa masoko maombi yatumwe kwa Makamu mkuu wa chuo Chuo cha Mafunzo Musoma Utalii S.L.P 1488- MUSOMA. Maombi yahusishe barua, wasifu binafsi, vyeti vya taaluma na cheti cha kuzaliwa vilivyo katika muundo wa PDF na vitumwe kupitia barua pepe/e-mail ya admissionmutc@gmail.com AU rashidmongomongo1@gmail.com .Kichwa cha habari cha barua pepe/e-mail kitaje nafasi husika.

**MWISHO WA KUTUMA MAOMBI TAREHE NI 20/09/2023 SAA 5: 59 USIKU**